



SIKU 16 ZA UANAHARAKATI 2023

MSHIKAMANO! UWEKEZAJI! HATUA THABITI!

MUHTASARI WA KAMPENI

○ Utangulizi

Kampeni ya Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia (UWAKI) ilianza mwaka 1991. Tangu wakati huo, inaadhimishwa kuanzia tarehe 25 Novemba ambayo ni siku ya Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na kumalizika tarehe 10 Desemba Siku ya Haki za Binadamu. Mtandao wa Kuzuia UWAKI umeshiriki kikamilifu katika kampeni ikiongozwa kwa kushirikiana na wanachama wake na kutoa kiti ya kuchukua hatua na Utetezi inayolenga kauli mbiu ya kikanda, kuhimiza uanaharakati kote katika Pembe ya, Mashariki, na Kusini mwa Afrika tangu mwaka 2004. Kwa zaidi ya miaka 30, wanaharakati kwa pamoja wamekuwa wakitetea haki na usalama wa wanawake na kujenga vuguvugu lenye nguvu kupitia Siku 16 za Uanaharakati. Tunapoanza safari ya mwaka huu, tunatoa wito wa kuwa na Mshikamano katika kuchukua hatua thabiti ili kuzuia ukatili dhidi ya wanawake.

○ Mshikamano! Hatua Thabiti! Uwekezaji! Katika kuzuia Ukatili dhidi wa Wanawake

Wanaharakati kutoka sehemu zote zilizo kwenye Pembe ya, Mashariki, na Kusini mwa Afrika wanajitahidi kuzuia Ukatili dhidi ya wanawake, kulinda haki za wanawake, na kuendeleza mabadiliko ya kijamii ya kifeministi. Ili kufanikisha mabadiliko ya kijamii ya kifeministi, ambayo yanahusu kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na kutetea stahili na usawa wa kijinsia, inahitaji kuwepo na mfumo mzuri wa kiekolojia unaohusisha wanaharakati, wafadhili, watunga sera, na watafiti.

Hata hivyo, katika miaka ya hivi karibuni, tumeshuhudia kupungua kwa nafasi ya mashirika ya kiraia kwa kiasi kikubwa katika utetezi wa mabadiliko ya kijamii ya kifeministi, katika kuhakikisha usalama, na kuzuia Ukatili Dhidi ya Wanawake. Kumekuwa na hali ya kutokukubalika kwa dhahiri kuhusu ajenda ya haki za



wanawake. Wapinga haki wanajipenyeza kwenye mashirika ya kiraia na taasisi za kidini na kuwatumia wanasiasa kupitisha jumbe zao. Pia wanatumia vitisho dhidi ya wapinzani wao wa kisiasa na kupotosha kwa kiwango cha hali ya juu na kutafuta uungwaji mkono kwa umma ili kuendeleza ajenda zao. Kuendela kwa hali hii yenye mtizamo hasi ni tishio kwa maendeleo ya ajenda ya kifeministi na yanaweza kusababisha kurudisha nyuma jitihada hizo.

Tunapoanza kampeni ya Siku 16 za Uanaharakati ya mwaka wa 2023, tunakualika uweze kuchunguza njia zinazoweza kuleta mshikamano katika kurejesha nafasi, na kuipa kipaumbele ajenda ya haki za wanawake ikiwa ni pamoja na kuongeza uwekezaji katika kuzuia Ukatili Dhidi ya Wanawake, ili kufanikisha kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake kwa kuwekeza katika hatua endelevu ili kuhakikisha uungwaji mkono kisiasa na utekelezaji wa mikakati ya ufadhili iliyo bora, na mikakati yenye taarifa zenye uthibitisho kutoka kwenye sekta mbalimbali.

Kwa pamoja, tunasimama tukiwa na sauti ya pamoja na kuwasilisha kwa nguvu na kuweka kipaumbele katika kushinikiza uwekezaji, na kuzuia kutokukubalika kunako weza kuturudisha nyuma.

Lengo la kampeni

Katika kampeni hii, tunaunganisha nguvu za pamoja, tukivuka mipaka na asili zetu, ili kutetea usawa wa kijinsia na haki. Kwa kushirikishana kwa pamoja uzoefu, ufahamu wetu, na uelewa, tunajenga mtandao thabiti wa usaidizi, na kukuza uhusiano usioweza kuvunjika ambao unatuwezesha wanawake kuinuka na kustawi kwa pamoja. Tunasimama kwa uthabiti dhidi ya hali ya kutokukubalika na mifuko ya upinzani kwa njia zenye matumaini yakistawishwa na kuingwa na mshikamano unaokubalika na watu binafsi, mashirika, na jamii inayotuunga mkono. Ili kuunda mshikamano huu, lazima tuungane kwenye lengo letu la pamoja na kujitoa kwa dhati kwenye vuguvugu la kifeministi.

Ili kufanikisha malengo haya, tunawaalika wanaharakati, mashirika na jamii kushiriki kama ifuatavyo:

Watu Binafsi:

Nguvu za wengi huanza na nguvu ya mtu mmoja! Hatua tunazochukua kama watu binafsi, zikiwa ndogo au kubwa, zinaweza kuwahamasisha wengine kufanya hivyo, na kuchochea mabadiliko. Hatua thabiti zinaweza kuwa za aina mbalimbali:

- Jiunganishe na uanaharakati wako wa ndani na wale ambao wanaunga mkono safari yako
 - a. Fikiria kuhusu uzoefu uliokupatia usaidizi ukiwa katika wakati ngumu.
 - b. Tafakari jinsi uzoefu huo ulivyokuongoza katika kutetea ustawi wako binafsi.
 - c. Andika uzoefu huo kama kumbukumbu.
 - d. Ikiwezekana, fikisha shukrani zako kwa wale waliokuunga mkono, au shirikisha hadithi yako kwa mtu unayetaka kujenga naye undugu ulio imara zaidi.
- Chukua muda kukumbuka na kuheshimu mfungamano huu maalum ambao ulikuwezesha kustawi.

Shirika la Wanaharakati/ Wafadhili

- Shinikiza changamoto za hali ya ushindani wa mfumo wa kiekolojia wa ufadhili kwa kuwa na ndoto na kujenga malengo shirikishi na wadau na mashirika yenye mreno wako.
- Sitawisha vuguvugu lenye moyo wa ukarimu katika kutafuta rasilimali kwa ajili ya kuzuia Ukatili Dhidi ya Wanawake.
- Toa nafasi ya makusudi katika shirika lako kwa watu ambazo sauti zao mara kwa mara hazisikiki
- Jadili mikakati ya kuimarisha makutano ndani ya vuguvugu la mabadiliko ya kijamii la kifeministi, kwa kuhakikisha uwepo wa mbinu jumuishi zaidi za haki na usawa wa kijinsia.
- Sherehekea mshikamano na urafiki ulioanzishwa ndani ya shirika lako, unaounganisha kila mmoja katika kutetea programu na uwekezaji ili kuzuia Ukatili Dhidi ya Wanawake.

Jamii

Ni kwa namna gani jamii yako inaweza kufanya uwekezaji wa pamoja katika kuzuia Ukatili Dhidi ya Wanawake?

- Anzisha sehemu salama katika jamii yako ambapo watu binafsi wanaweza kushirikishana hadithi zao, mitazamo na uzoefu wao, wakikuza uelewa na ufahamu.
- Anzisha midahalo itakayowaunganisha watu tofauti, na kushirikiana katika harakati
- Wezesha jukwaa litakalo himiza uelewano miongoni mwa wanajamii.
- Imarisha ustawi wa watu wote ndani ya jamii yako.
- Sherehekea mfungamano wa usaidizi ndani ya jamii, katika kutetea na kuzuia Ukatili Dhidi ya Wanawake.

Mshikamano na kuchukua hatua thabiti unalenga kuunganisha watu, kutoa usaidizi, kufungamanisha na undugu wakati tunapotetea ukweli bila ya Ukatili. Kwa kuwekeza katika ufadhili, afua mbalimbali, programu za kijamii, uungwaji mkono kisiasa, na sera zilizoimara, tunaweza kustawisha ulimwengu ulio salama kwa pamoja.

Chunguza kiti yetu, iliyoandaliwa ili kushirikisha watu binafsi, mashirika na jamii. Fanya uchaguzi kulingana na muktadha wako, ukizingatia hali yako ya upekee, lugha iliyo rahisi kueleweka ambayo inasisitiza umuhimu wa kuwekeza katika kuzuia Ukatili Dhidi ya Wanawake. Kwa pamoja, tusimame imara, tukiwa na sauti ya pamoja, na kuazimia katika kuchukua hatua thabiti, huku tukilisukuma nyuma wimbi la upinzani na kujenga mustakabali wa siku zijazo bila Ukatili Dhidi ya Wanawake.